# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara yaChukwani, Buyu,
70490 MjiniMagharibi,
S.L.P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 2242000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA UTALII, BIASHARA NA KILIMO YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUANZISHA TAASISI YA UTAFITI WA UVUVI NA MALIASILI ZA BAHARINI ZANZIBAR NA KUWEKA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO.

**Mheshimiwa Spika,**

Awali ya yote napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, mwingi wa rehema na mwenye kurehemu, kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii ndani ya Baraza letu tukufu kuendelea na majukumu yetu ya Kitaifa. Namuomba Mola wetu anijaalie ufasaha katika uwasilishaji wa Hotuba hii na atupe usikivu na uelewa ili tuweze kuuchangia kwa umakini wa hali ya juu na hatimae kuupitisha mswada uliopo mbele yetu kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa namna ya pekee napenda kuchukua fursa hii adhimu kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niwasilishe maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na **"Mswada Wa Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo".**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inatoa pongeza za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa ujasiri wake katika jukumu zima la uongozi wa Nchi hii, sambamba na jitihada anazozichukua za kuendeleza sekta ya uchumi wa Buluu kwa vitendo kwa kuhamasisha matumizi bora ya rasilimali za baharini na kufanya jiitihada ya kuongeza thamani ya mazao hayo ili kuweza kumkomboa mwananchi wa Zanzibar kuichumi na kuweza kubadilisha hali za maisha za wananchi wetu kupitia sekta hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba sasa nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi Mh. Suleiman Masoud Makame pamoja na timu ya watalaamu wa Wizara pamoja na wale wanaotoka katika Taasisi ya Utafiti (ZAFIRI) kwa mashirikiano yao waliyoipatia Kamati yetu katika kipindi chote cha majadiliano ya Mswada huu.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kuwashukuru Wanasheria wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa uchambuzi na ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizojitokeza wakati wa kuujadili mswada huu kwenye ngazi ya Kamati. Michango yao ni muhimu katika kuujenga mswada wetu kwa maslahi mapana ya nchi yetu na watu wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Natoa pongezi za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Utalii, Biashara, na Kilimo kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuujadili na kuuchambua mswada ulioletwa mbele yao kwa upeo na ustadi wa hali ya juu. Naomba sasa niwape fursa Wajumbe wa Baraza hili kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii mmoja baada ya mwengine kama ifuatavyo:

1. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Mwenyekiti
2. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - M/Mwenyekiti

3. Mhe. Said Saleh Salim - Mjumbe
4. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Mjumbe
5. Mhe. Mihayo Juma Suleiman - Mjumbe
6. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Mjumbe
7. Mhe. Suleiman Makame Ali - Mjumbe
8. Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi - Katibu
9. Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi - Katibu
10. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu

**Mheshimiwa Spika,**

Mswada huu unalenga kukuza utafiti katika maeneo ya uvuvi, Maliasili za Baharini, ukuzaji wa viumbe maji pamoja na sayansi ya baharini ndani ya Zanzibar kwa kuanzisha Taasisi ya utafiti yenye lengo mahsusi la kufanya tafiti bora na zenye viwango ili kuwezesha Maliasili za Baharini kuwa endelevu pamoja na kusaidia shughuli za uvuvi kufanyika kwa weledi mkubwa bila ya kuathiri Maliasili zilizomo ndani ya bahari.

Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii nzuri kwa vile Zanzibar tunatekeleza Sera ya Uchumi wa Buluu kwa vitendo. Hivyo basi, uwepo wa Taasisi hiyo utapelekea kuleta tija katika kutoa elimu kwa wavuvi, wafugaji wa samaki na wakulima wa mazao ya Baharini juu ya namna bora ya kutumia Maliasili za Baharini katika kujiinua kiuchumi kupitia Sekta hii ya Uchumi wa Buluu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu imefanya marekebisho kadhaa kwenye mswada huu yakiwemo marekebisho ya herufi, kuongeza tafsiri ya maneno ambayo hayajatolewa ufafanuzi katika mswada wa Kiswahili, kufuta maneno, kuondoa makosa ya

kisarufi na kuweka uwiano baina ya nakala ya mswada wa Kiingereza na Kiswahili yanayoonekana kwenye waraka wa mapendekezo ya marekebisho ambayo yameingizwa katika mfumo wa Baraza Mtandao. Kimsingi, Kamati imeridhika na maudhui, dhamira na malengo ya mswada huu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imefanya marekebisha katika kifungu cha 3 (2) kwa kuingiza maneno **"kwa kuzingatia Sheria husika"** baina ya neno **"Taasisi"** na **"Itakuwa"** na kusomeka **"Taasisi kwa kuzingatia Sheria husika itakuwa ni chombo kinachojitegemea.** Marekebisho haya yataleta maana kuwa kifungu kidogo 2(a-e) vitatekelezwa kwa mujibu wa Sheria husika tofauti na ilivyokuwa imesomeka hapo awali ambapo kifungu kimoja tu cha 2(d) ndicho kingeliweza kufuata sheria katika utekelezaji wake jambo ambalo lingepelekea kutoa mwanya kwa watendaji ambao si waaminifu kutumia fursa hii kwa kutekeleza majukumu yaliyoanishwa katika kifungu kidogo 2(a-e) kinyume na na sheria husika kutokana na mapungufu hayo wakati wa utekelezaji wa Sheria hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imeendelea kufanya marekebisho kwa kuongeza kifungu cha 35 (1)(2) chenye "Marginal note" (kufuta na kubakiza) kifungu ambacho kitatoa fursa ya kufuta sheria ya awali ambayo imeanzishwa kwa **"Legal notice"** ya Mh Rais, na kutoa uhalali wa kutumika kwa Sheria hii. Kimsingi, kifungu hiki kilikuwa hakipo katika Mswada huu.

Kamati imependekeza hili ili kufuata miongozo na taratibu za uandishi wa Miswada ya kisheria aidha kuzuia matumizi ya sheria ya awali baada kupitishwa kwa sheria mpya ili kuepusha mgongano wa sheria mbili kutumika kwa wakati mmoja katika jamii na kuepusha migogoro isiyokuwa ya lazima.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile Kamati imefanya marekebisho katika kifungu cha **30 (1)(b)** kwa kufuta neno **"ambayo"** na kuweka maneno **"ya faini yaliyoainishwa kwa kuzingatia kosa alilolifanya"** na kifungu hiki kusomeka **" atalipa malipo yote ya faini yaliyoainishwa kwa kuzingatia kosa alilolifanya chini ya Sheria hii.**

Kamati imeona ni vyema kufanya marekebisho ya kifungu hiki ili adhabu na faini zitolewe kwa ukamilifu wake kulingana na kosa husika.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kumalizia, natoa shukurani za dhati kwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa utulivu na usikivu wao wakati wote wa uwasilishaji wa taarifa yetu na naomba tuuchangie, tuujadili, tutowe mapendekezo na hatimae tuupitishe mswada huu ili kuimarisha sekta ya uvuvi na yenye kuleta tija kwa jamii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba ya Kamati yangu, naomba kuwasilisha.

……………………

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf,
Mwenyekiti,
Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**